## KOZI YA MSINGI YA WAVUMBUZI KWA MASTER GUIDE MAFUNZONI

## I: HISTORIA, FALSAFA, NA_MADHUMUNI

HISTORIA:

Chama cha Wavumbuzi kilianzishwa rasmi mwaka 1939.

FALSAFA:

Chama cha Wavumbuzi ni huduma huru iliyodhaminiwa na Kanisa la Waadventista Wasabato kwa watoto wenye umri wa miaka 6 - 9, ambapo kanisa, familia na shule huungana pamoja kuwasaidia watoto kukua kwa furaha katika hekima na kimo wakimpendeza MUNGU na wanadamu.

Chama cha Wavumbuzi husaidia wazazi katika kufanya maendeleo ya watoto wao kuwa ya thamani na maana.


### MAELEZO YA MUHIMU KUHUSU MALEZI

Kushirikisha Wazazi na kuwapa watoto nafasi ya kujifunza na kupata uzoefu katika haya:

- Maisha ya Kiroho, Kiakili, Kimwili, na Kijamii.
- Kwamba mtoto aweze kulisaidia kanisa lake anapojitambua yeye ni sehemu ya kanisa
- Mtoto ajitambue na kujithamini kwamba yeye ni sehemu ya jamii inayomzunguka.
- Kuongeza na kuimarisha uhusiano kati ya mtoto na mzazi wake, na kumkuza mtoto Kiroho, Kimwili, Kiakili na Kijamii.

#### MAWAKALA WANAOCHANGIA MALEZI YA MTOTO

- Mawakala hawa wanaweza kuchochea malezi mazuri ama malezi mabaya.



- **Jedwali linaloonesha uhusiano wa mawakala wa malezi ya mtoto**

**MADHUMUNI YA CHAMA CHA WAVUMBUZI**

Chama cha Wavumbuzi kinatoa furaha na njia za ubunifu kwa watoto.

1. Kujenga tabia ya KRISTO ndani yao.
2. Kuizoea furaha na kuridhika kwa kufanya mambo mema
3. Kuonesha upendo wao kwa YESU kwa njia za asili
4. Kujifunza michezo mizuri na kuimarisha uwezo wao na kuwa karibu na wengine
5. Kugundua vipawa walivyopewa na MUNGU, kujua namna ya kuvitumia ili kuwasaidia wao binafsi na wengine pia.
6. Kugundua dunia/ ulimwengu wa MUNGU
7. Kuimarisha uelewa wao juu ya mambo yanayoifanya familia kuwa imara
8. Kuendeleza msaada kwa wazazi kwa njia ya mafunzo ya watoto.

## II. MUUNDO WA CHAMA:

## A: JINSI YA KUANZISHA CHAMA

1. Uwe na njozi - Mpango wa mbele utafanya nini.
2. Soma Biblia, Roho ya unabii, Kanuni ya Kanisa.
3. Soma miongozo ya wavumbuzi.
4. Shauriana na Mchungaji kwa njozi ulizo nazo.
5. Ita mkutano wa wazazi zungumza umuhimu wa mtoto kuwa ndani ya chama na hasara ya kutokuwepo ndani ya chama.
    - Taratibu za kujifunza, waone utofauti watakaokuwa nao kwa wengine kwa kuwa na sare.
    - Kutakuwa na ziara mbalimbali, muda wa kukutana na watoto.
6. Andaa mahubiri juu ya malezi ya watoto, onyesha mifano ya watoto wa Biblia.
7. Andaa sherehe za uzinduzi
8. Fanya tathmini

**B: UONGOZI: Kuna viongozi wa aina mbili:**

1. **Viongozi wanaochaguliwa na Kanisa**
   i. Mkurugenzi (awe Master Guide)
   ii. Mkurugenzi Msaidizi (Master Guide/Mafunzoni)
   iii. Katibu/ Katibu Mhazini
   iv. Mshauri
   v. Mzee wa kanisa/MChungaji
   vi. Mzazi anayewakilisha wazazi wengine
2. **Viongozi wanaochaguliwa nza wanachama wenyewe**
   i. Waalimu (viumbe, tuzo, madarasa, michezo n.k)
   ii. Washauri
   iii. Waelekezaji

## C: MADARASA YA WAVUMBUZI

| No: | JINA LA DARASA | UMRI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUKI WA SHUGHULI | MIAKA 6 | Wana shughuli nyingi, si watulivu |
| 2. | MWALI WA JUA | MIAKA 7 | Wanaanza kuchomoza |
| 3. | MJENZI | MIAKA 8 | Kujenga tabia |
| 4. | MKONO WA MSAADA | MIAKA 9 | Anaelewa mambo anaweza kutumika/kutumwa |

## D: SIFA ZA KIONGOZI ANAYEFAA KUWALEA WATOTO.

### Kutoka 18:1 -

i. Ampende Mungu kwa kiwango cha juu. (Awe mtu wa Kiroho)
ii. Awapende watoto kwa vitendo.
iii. Awatumikie kwa moyo na Kipawa Kinachotamaniwa na Mbingu.
iv. Awe mwenye kutawala hisia, kujiheshimu na kuwa na kiasi.
v. Apende mambo ya nje, kwa kuwa ndizo shughuli za watoto zilizo nyingi.
vi. Ajue tabia za watoto.
vii. Mwenye kujielimisha katika fani mbalimbali, ajifunze kutoka kwa wengine. *(Mwenye kupenda kusoma vitabu na kutafiti mambo)*
viii. Mwenye uwezo wa Kuongoza (Kiongozi Bora).
ix. Awe na malengo makubwa aanze na yaliyo rahisi.
x. Agawe Madaraka, anaewandaa wengine kuwa kazini / viongozi
xi. Mwenye uhusiano mzuri na wengine.

xii. Anaekubali mambo mapya.
xiii. Be resourceful and resource

## E: WIMBO WA CHAMA, AHADI NA SHERIA

**WIMBO:**

**AHADI:** Kwa kuwa YESU ananipenda, nitafanya vema kila wakati.

**SHERIA:**

1. Be obedient
2. Be pure
3. Be true
4. Be kind
5. Be respectful
6. Be attentive
7. Be helpful
8. Be cheerful
9. Be thoughtful
10. Be reverent

## F: SERA ZA CHAMA

1. Sare
2. Mambo ya fedha
3. Taarifa

## KUWAELEWA WAVUMBUZI.

Tabia za wavumbuzi zimewekwa katika hali ya Kimwili, Kiroho, Kiakili, Kijamii na Kihisia, Tutaangalia tabia za jumla.

**A: Tabia za jumla za Watoto.**

i. Umri wenye shughuli nyingi
ii. Wanapenda mambo ya kukariri na chemsha bongo, kuimba na hadithi nzuri zinazowasisimua au kuwatia moyo.
iii. Wanapenda Michezo na burudani

iv. Ni watiifu na waaminifu, husema kweli daima, na hawajui kusema uongo.
v. Hupenda kutumwa sana, hufanya kazi kwa kushindana, na kazi zao hupenda zihakikishwe na mtu mzima.
vi. Hupenda kutembea wenye jinsia moja.Hupenda marafiki
vii. Ni umri wenye kupenda sifa.
viii. Wanatunza kumbukumbu sana, lakini pia huweza kusahau
ix. Ni wadadisi sana wa mambo mbalimbali, ni wafikiriaji wazuri na huuliza maswali.
**x. Huamini kila kauli ya Mwalimu**
**xi. Imani yao iko kwa Mzazi kuliko kwa Mwalimu**
xii. Wana ubinafsi, Wana ubaguzi.
xiii. Wana kimbelembele.
xiv. Wanakata tamaa mapema.
xv. Wanaiga kila kitu. *(hawana uwezo wa kupambanua jema na baya)*
xvi. Wanahisi hatari kwa kuona uhalisia wa mtu au kitu. Mfano mwalimu akikasirika au kufurahi.
xvii. Ni waoga wa vitu au mambo ambayo hawajayazoea.
xviii. Wanahitaji kupendwa sana na kuthaminiwa

**Mwalimu unapaswa kufanya nini:**

i. Wafundishe kuzitumia nguvu walizonazo kwa kufanya majukumu unayowapatia. Mfano, kuimba kwa vitendo, kukariri mafungu, kufanya kazi za kanisa n.k
ii. Wafundishe hadithi za Biblia kwa bidii na uwashawishi wazitumie maishani.
iii. Kuwa rafiki yao
iv. Wape nafasi ya kuonesha wanayojifunza mbele za wazazi wao
v. Watie moyo katika kazi zao wanazofanya na uwaelekeze kwa umakini na upendo.
vi. Kuza talanta na vipaji vyao

## B: JINSI YA KUSHUGHULIKIA WATOTO WENYE MATATIZO MAALUM

### ❖ Kuna makundi maalum manne ya watoto:

**I. Watoto wenye Matatizo ya akili ilyovia/ iliyodumaa:**

**Sababu:-**

- Lishe duni.
- Malezi ya Wazazi.

- Upweke.
- Kutothaminiwa

**Jinsi ya kuwasaidia:-**

- Fanya urafiki nao.
- Waketishe karibu nawe unapofundisha
- Usiende polepole wala haraka mno unapofundisha.
- Wapangie muda wa ziada wa mafundisho kwa ajili yao.

### II. WATOTO WATUKUTU.

**Sababu:**

i. Mifarakano katika familia
ii. Kuachana au kusambaratika kwa familia.
iii. Malezi mabovu

**Jinsi kuwasaidia:-**

- Fanya urafiki nao
- Waketishe karibu nawe.
- Waombee watoto ukiwa nao.
- Shirikiana na wazazi/walezi katika kuwasaidia

### III. Waliopata hasara kubwa

**Sababu:**

i. Kufiwa na Wazazi (ni yatima)

**Jinsi ya kuwasaidia:-**

- Uwe nao karibu.
- Elewa mahitaji yao.
- Wapatie nafasi ya utumishi. *(mfano; kuomba, kutumwa kazi, kuongoza ibada n.k)*

## IV. Watoto walio wepesi kuelewa/ Wenye vipaji

**Sababu:**

- Ndivyo walivyozaliwa ama kulelewa

**Jinsi ya Kuwasaidia.**

- Kuza vipaji vyao:
- Watawanye darasani.
- Watumie kuwasaidia wenzao.
- Mshirikishe katika mipango.

## C: NIDHAMU KWA MTOTO

Ni hali ya kumfanya awe na furaha na mwanadamu kamili hapo baadaye, ni Maadili yanayomsaidia mtoto kujitawala na kujitambua.

**Ili awe na Nidhamu:-**

- Uwe mfano wa tabia.
- Jenga Mazingira yenye kuleta utulivu ili uvute usikivu wa Mtoto.
- Wabadilishie Mahali pa kujifunzia, na Waalimu wa Kufundisha.
- Maandalizi ya Mwalimu (Vifaa, soma mtaala uuelewe vizuri na uwe mbunifu.
- Weka malengo, washirikishe, utekelezaji wake liambie Kanisa.
- Kusahihisha makosa wakati wote na ukemee kwa mamlaka.

**Namna ya kuadhibu:**

1. Ongea na mtoto kama mzazi wake
2. Mweleze kosa lake
3. Usimseme mbele ya wenzake
4. Inapobidi mwadhibu mbele ya wenzake kuleta fundisho
5. Lengo la kuadhibu ni kuongoa Roho na si kuingamiza
6. Mtie moyo kwamba YESU anampenda, kwa kuwa anawapenda wadhambi
7. Omba naye

**Mafungu ya Biblia:** Mithali 22:6, Waamuzi 13:3-5, Mithali 1:10, Kumbukumbu la Torati 6:4-9, Mithali 16:25, Mithali 23:13-14, Mithali 22:15, Mithali 13:24, Mithali 19:18

## KUANDAA PROGRAMU ZA AC

Kuwaandaa watoto kujenga urafiki na Yesu,Kuwaelekeza katika umilele.

- Programu za mwaka(ndefu).
- Programu za robo au kila wiki.
- Programu za madarasa, kuonana na wazazi au ziara mbalimbali, mahubiri na uvishaji pini.

**Ili kufanikisha program hizi:-**

- Viongozi wawe na mipango.
- Watekeleze kalenda ya matukio.
- Washirikishe wakuu wa Kanisa katika Mipango.

## FALSAFA YA PROGRAM ZA WAVUMBUZI

Program zinazofundishwa kwa kutumia uzoefu na mtaala wa Wavumbuzi hukuza utii na uwajibikaji kupitia Nyanja za Kimwili, Kiakili, kiroho, na Kijamii

### I: KIMWILI

i. Stadi au kazi za nyumbani kama kutandika kitanda, kuosha vyombo, Usafi wa nyumbani, kufua nguo, kupiga pasi, kupika, kupanga meza, kutunza bustani.
   - Pia atumie ujuzi huo katika ziara za mafunzo, na picnic za familia

**II: KIAKILI:** Program iwe rahisi, isiwe ya mashindano, isiyoumiza kichwa tena iwapatie uzoefu wa kuona uwe mwingi zaidi

### III: KIJAMII:

- Iwasaidie wavumbuzi kupeana vitu mfano mwanasesere, chakula n.k
- Wafundishe kujifunza kukubali matokeo, na waishi na wenzao vizuri bila kuzingatia kilichotokea.
- Kuwa wenye adabu na ukarimu

**IV: KIROHO:** Kukariri mafungu, Chemsha Bongo, Kuelewa hadithi za Biblia kuimba nyimbo.

**V: UINJILISTI:** kutembelea wagonjwa nyumbani mwao, kuhudumia wazee na kujua kushukuru.

# MTAALA WA WAVUMBUZI.

Mtaala wa Wavumbuzi umegawanyika katika Mambo makubwa matano yenye vipengele vitatu kila moja;

1. **Mahitaji ya Msingi:-**
    - Utayari (Umri).
    - Majukumu(Kutumika).
    - Vichocheo(shime au tia moyo).
2. **Mungu wangu:-**
    - Mtoto aone kuwa Mungu ni wake (Kumwonyesha mfano wa Uumbaji, Wokovu ni wake, kuja kwa Yesu mara ya pili).
    - Ujumbe wa Mungu kwangu (Akariri Mafungu)
    - Kile ambacho Mungu anataka nitende (kwenda Kanisani, kutoa sadaka).
3. **Mimi mwenyewe.**
    - Ajigundue kuwa yeye ni wa pekee.
    - Agundue kuwa yeye anaweza kufanya uamuzi wa busara.
    - Agundue kuwa yeye anaweza kutunza mwili wake(Usafi,Mazoezi,Kiasi na muda wa kulala).
    - Kuheshimiana Kijinsia.
4. **Familia Yangu:-**
    - Ajue kuwa ni mmoja wa familia,nini sehemu yake nyumbani.
    - Ajue kuwa familia inajali kila mmoja ili aondoe ubinafsi.
    - Kusaidia kujijali (Usalama wake, wasifunge mlango mpaka arudi)kujijali na uwakili.
5. **Ulimwengu wangu:-**
    - Aelewe kuwa ulimwengu aliomo ana Marafiki,wazuri na wabaya.
    - Kuna watu wengine hawafanani (weupe na weusi) wapole na wakorofi, Kanisani na Barabarani na Shuleni.
    - Asili ya ulimwengu huu.

**JINSI YA KUWAFUNDISHA**

- Kulipenda neno la Mungu.
- Kulipenda kanisa la Mungu.( Kulijali).
- Waandaliwe kwa huduma(nyumbani na kanisani, kutenda kazi.

**Anamsikia Mzazi:-**

- Kuwashirikisha Wazazi ili kurahisisha ufundishaji.
- Washirikishe wazazi kile utakachofundisha (sheria).
- Wape wazazi vitu vya kufuatilia.

- Wape uhuru wazazi wajieleze tatizo alilonalo mtoto.
- Waambie wazazi matatizo waliyonayo watoto.

## Hatua za ufundishaji:-

1. Anza na Mpango mzuri.
   - ✓ Uwe na ratiba ionyeshe mada na vipengele.
   - ✓ Ni mara moja au mbili kwa wiki nani Dk 20 tu.

***Mfano:-***

| Mada Kuu | Mada ndogondogo | Muda | Kazi | Idadi ya watoto | Tathmini |
|---|---|---|---|---|---|
| Kurudi kwa Yesu | Dalili au Matayarisho | Dk 20 | Zoezi | 25 | Somo limeeleweka |

2. Elewa mahitaji yao:-
   - Yaelewe vizuri na jinsi yanavyoweza kutosheleza Malengo yako.
   - Katika robo hii unataka wapate nini (lengo).

3. Fikiria watoto wako.
   - Je mahitaji yao ni nini, Wanapen delea nini.
   - Je ni mambo gani ambayo wameshayafahamu.
   - Anza na mambo rahisi au yaliyojulikana.
   - Je hitaji hilinninalowafundisha litawasaidiaje.

4. Amua kile ambacho ni lazima kifundishwe :-
   - Weka kipaumbele,tafuta ambacho ni cha muhimu.
   - Panga hatua uwasaidie.

5. Panga kazi ya darasa:
   - Rudia uone una vipindi vingapi na utatumia muda gani kumaliza mada.

6. Panga ratiba.
   - Hakikisha kuwa kila kipindi kiwaongezee watoto kuelewa.

❖ **Kumbuka:** Watoto ni wepesi kuchoka, kipindi isizidi dakika 30, na unapofundisha zitumie kwa kuchanganya mambo, nyimbo, mazoezi kidogo n.k

**NAMNA YA KUFUNDISHA.**

1. Amsha hamu, kwa kutumia picha, hadithi, vitu halisi au matendo, kadiri inavyowezekana wafanye watoto wagundue wenyewe, alika wageni, mjadala na picha.

2. Washirikishe katika kutenda, ndivyo anavyoelewa haraka ni njia ya kupima uelewa wao (zoezi).
    - Nyimbo za vitendo, Michezo na maswali.

3. Fanya tathmini kagua kazi zao.

4. Kusanya Maarifa:- Vitabu rejea, Ziada visivyo katika Miongozo,
    Kiada vilivyo katika Miongozo, na Hudhuria semina mbalimbali zinazohusu mambo ya vijana.

5. Fundisha mtoto na siyo darasa, litawale darasa.
    - Tathmini darasa na jiulize maswali haya.
    - Je somo hili limewasaidia watoto.
    - Je kusudi la somo hili limewasaidia watoto.
    - Je ni vitu gani nilivyofanya.
    - Alika Mwalimu au mtu akusikilize na akupe tathmini na urekebishe ulipokosea.

**MTANDAO WA FAMILIA YA WAVUMBUZI:-**

- Uwe na vikao au na mikutano na wazazi.
- Katika ziara uwe na wazazi au walezi wao, wavumbuzi katika umri wao ndipo wanapoanza kuvumbua vitu mbalimbli, na ikumbukwe kwamba kwao kila kitu ni kigeni.
- **Kumbukumbu la Torati 4:6-9; Waebrania 11:7.**

**Umri miaka 0-9**

- ❖ Ni umri unaofaa kumjengea mtoto tabia.
- ❖ Wazazi na Kanisa ndio walimu.
- ❖ Kila kitu kwao ni kipya.

## Unapofundisha Zingatia:-

i. Fundisha dini, Kichwani mwake awe Yesu tu. Jinsi ya Kumheshimu Mungu, tangu utoto ajue namna ya kuomba na kupiga magoti.
   - Tafuta muda ambao akili hazijachoka
   - Fundisho liwe fupi. (Dk 20).
   - Lifanye somo liwe fupi na la Kupendeza kwa kulingana nao na kufanana nao.
   - Badilisha mtindo wa ibada au kujifunza Usiwe na staili ileile tu kila siku, ili wasione ibada kama kitu kisicho na maana.

- **Dini ipi wanapaswa kufundishwa; Yakobo 1:27, Mathayo 22: 37 – 40, Kumbukumbu la Torati 6: 4 - 9**

ii. Wafundishe kuishi maisha ya kiasi. Tabia ya umimi (changu) kujipendelea iondoke.

iii. Kuepuka mazoea mabaya.
   - Umri huu wanaingia katika mazoea mabaya kirahisi kwani hawawezi kupambanua mema na mabaya.
   - Aina ya chakula vinywaji vinachangia kuwa na mazoea mabaya, hivyo watenganishiwe.

iv. Wafundishwe kujihusisha na kanisa (Waebrania 10:25).

v. Jenga mahusiano mazuri kati ya Mzazi, Kanisa na mwalimu. (Watembelee)

vi. Fundisha heshima na utii. Kutoka 20:12, Mambo ya walawi 19:32.
   - Picha ya watoto ndio itakayodhihirisha tabia ya Mwalimu.

vii. Wafundishe watoto kufanya kazi kwa juhudi, Kuwaacha watoto kukua kivivu ni dhambi. (Zungumza na Wazazi ) Mithali 14:23; 16:26 katika kazi. Kutoka 20:8, 2Wathesalonike 3:10 - 12

viii. Wafundishe watoto kujali elimu( Mithali 4;13) Kanisa lianzishe shule ya chekechea.

## Adventurer Types of Uniform

## Class "A" Uniform for the Adventurer boy and girl

**GIRLS:** Navy blue pinafore or skirt, white blouse (shirt type blouse with short sleeves).

**BOYS:** Navy blue pants, white shirt with short sleeves and regular collar.

**BOYS/GIRLS:** Shoes: uniform within club; Navy blue or white socks: uniform within club.

**SCARF:** Adventurer scarf is part of the uniform worn with an Adventurer slide.

**AWARD SASH:** The sash is navy blue and part of uniform.

## Class "A" Uniform for Adventurer Staff

**LADIES:** Navy blue A-line (slim) skirt; White blouse (shirt type blouse with short sleeves)

**MEN:** Navy blue pants, white shirt (with short sleeves and regular collar)

**MEN/LADIES**: Shoes: uniform within club; belt: uniform within club; Navy blue tie (optional for men)

**SCARF:** The Adventurer scarf is part of the uniform and worn with an Adventurer slide. Staff members who are Master Guides may wear their Master Guide scarves

**SASH:** Sash is navy blue and worn at appropriate times. A Y honors are NOT to be worn on the Adventurer sash; only Adventurer awards are to be worn on sash.

**EMBLEMS:** Adventurer Patch, place on right sleeve
Adventurer World, place on left sleeve
Club Crescent, place on right sleeve above Adventurer patch
**Adventurer Awards**, worn on the sash
**Class Pins**, worn on shirt or blouse pocket

**Field Uniform (Type B)**


Field uniform for the Adventurers and staff is a T-shirt and blue jeans. Each club may create its own design for field uniform T-shirts and sweatshirts. A few suggestions for designs on T-shirts are:

i. Adventurer logo
ii. Local club logo
iii. Adventurer and local club logo

**INSIGNIA PLACEMENT**

**LEFT SLEEVE**

The Adventurer World emblem is to be worn on left sleeve 1½" below the shoulder seam.



Left Sleeve

**RIGHT SLEEVE**

The Adventurer Club Name Crescent is to be worn ½" below the shoulder seam. The Adventurer Club Emblem is to be worn 2½" down from the shoulder seam.




Right Sleeve

**SASH**

Adventurer awards and class pins, only. If you have earned any AY/Pathfinder Honors you are not to place them on your sash.

**NAME TAG**

Your name tag is to be centered over the right pocket or its equivalent position on the sash or blouse.

**STAFF**

Your staff rank stripe goes between the club name crescent and the Adventurer Club Emblem. Move the Adventurer Club Emblem down an extra inch.

You are to wear an Adventurer sash ***(not an AY/Pathfinder sash***) even if you are a Master Guide.

**EMBLEM**

**Adventurer World Logo**

**Adventurer emblem**

END